# BUNAMFAN CLUSTER EXAMINATION - 2022

**Kenya Certificate of Secondary Education**

# 102/3 – KISWAHILI – Paper 3

**(FASIHI)**

## June 2022 - 2 ½ hours

**Name**.......................................**Adm No**......

**Class**............... **Date**...............................

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(c) Jibu maswali **manne** pekee.*

*(d) Swali la **kwanza** ni la **lazima**.*

*(e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani:*

*Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi*

*(f) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.*

*(g) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| **Swali** | **Upeo** | **Alama** |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | **Jumla** | |

**SEHEMU A**

**USHAIRI**

**1.** ***Lazima***

**Monyara**

Nakumbuka kwa dhiki Mto Monyara
Tuliochelea kukaribia kingo zake
Tukatulia kwanza; ukakamavu kujihamia
Kwa kunyenyekea  wingi wa yake maji
Yaliyojiendea utadhani yamesimama.

Ni katika mto huu
Ambapo samaki wakubwa tulivua
Maguo kuyatakasa japo kwa kunyemelea
Na walevi stadi wakachelea kuuvuka
Ulipofura na kupita kwa kiburi
Kwa kushiba maji yake
Yaliyofanya mawimbi madogo.

Ni hapa ambapo marehemu nyanya
Mkono alinishika na njia kuniongoza
Juu ya ulalalo wa miti
Vikapu vyetu hewani vikielea;
Mimi nikishika changu kwa mkono mmoja
Naye akikiachilia chake kujishikisha kichwani
Masafa baina yetu na mtambo
Uliokwenda kwa maji
Tuliyapunguza kwa kila hatua tulopiga.

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

Ni katika mto huu ambapo
Samaki tuliowavua tuliwapasua na kuwasafisha
Na hivyo kuuficha umaskini wetu
Ulotuzuia kununua mnofu wa bucha
Ni hapa ambapo wanawake walifika
Mawe ya kusagia kupata
Ni katika mto huu ambapo
Waumini walifika kutakaswa kwa ubatizo
Baada ya ulevi, uzinzi na kufuru nyinginezo.

Ni hapa ambapo ilisimuliwa kuwa
Hata wachawi walifika kufanya vitimbi vyao
Baada ya utawala wa jua kumezwa na nguvu za giza
Sasa Monyara nilioijua haipo tena
Zimebaki kingo zilizokaukiana
Kama uso wa mrembo aliyekosa mafuta
Siku ayami.

Mto huu ambapo pembeni mwake
Watoto walipashwa tohara
Maji yake yakishangilia, umekonda
Na mbavu zake nje kutoa
Na sasa vitoto vikembe vinazikanyaga
Vikijiendea zao kusaga mahindi
Juu mlimani
Katika mtambo wa Kizungu
Usioisha kulalamika
Nao wanawake hawaji tena
Kutafuta mawe ya kusagia wimbi

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

Imebaki njia ya walevi warejeao nyumbani

Nayo miti iliyosimama wima ukingoni

Iliisha kuanguka kwa kuleweshwa na pumzi za walevi

Wasioisha kupita hapa.

(a) Onyesha umuhimu wa Mto Monyara kwa wanakijiji. (alama 4)

(b) Toa mifano ya mishata inavyojitokeza shairini. (alama 2)

(c) Eleza aina **tatu** za taswira zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 3)

(d) Fafanua mtindo katika shairi hili. (alama 3)

(e) Tambua nafsi neni ya shairi hili. (alama 1)

(f) Jadili idhini ya kishairi katika shairi. (alama 3)

(g) Andika ubeti wa pili katika lugha nathari (alama 2)

(h) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**SEHEMU YA B**

**Riwaya**: *Chozi la Heri* - Assumpta Matei

Jibu swali la *2 au 3*

**2.** "Wapo baadhi yetu ambao wizi unapotokea inasemekana wanashirikiana na wahalifu wenyewe na baadaye wanagawana ngawira nao!"

***a)***

i) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

ii) Jadili mtindo katika dondoo hili (alama 3)

iii) Eleza sifa za usemaji wa dondoo hili (alama 3)

***b)*** Ufisadi unaojadiliwa katika dondoo una madhara katika jamii ya Wahafidhina. Jadili. (alama 10)

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**3.**

***a)*** Jadili mtindo kwenye dondoo hili. (alama 8)

Jua linalochomoza halina ule wekundu wa jua la matlai ambao huleta haiba ya uzawa wa siku yenye matumaini. Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua. Tukio hili linafuatwa na umeme, kisha mtutumo wa radi. Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua; matone yanayoanguka kwenye ngozi laini za wanangu wakembe, Lime na Mwanaheri. Nawatazama kwa imani lakini siwezi kuwasaidia. Sina hata tambara duni la kuwafunikia. Linalobaki ni kumshuru Mungu kuwa tungali hai. Ubavuni mwangu amelala maskini mke wangu,Subira. Sijui kama inahalisi kumwita mke wangu kwani huyu siye Subira wangu wa zamani. Siye, siye, siye-e-e-e. Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha, kikwi. Tazama tambo lake lililoumbuka. Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira. Lakini yeye hana la hamira! Haya ni matokeo ya ubahaimu wa binadamu. Kwa mbali namwona Ridhaa – mwamu hasa – akitafuna kitu fulani, nadhani ni mzizimwitu. Ridhaa, kweli Ridhaa kula mzizi! Daktari mzima! Mkurugenzi mzima wa Wakfu wa Matibabu

nchini! Wanasema wajuao kuwa simba akikosa nyama hula nyasi. Msafiri kafiri ati! Amekosa la maama, hili la mbwa ataliamwa!

***b)*** "Huyu hapa ni Bwana Mwangemi na huyu hapa ni Bi Neema. Kama nilivyokujuza hapo awali, wamekuja kuchukukua kwenda kuishi nao kama mwana wao."

i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii) Banaisha mtindo katika dondoo. (alama 3)

iii) Toa sifa za msemaji wa dondoo hili. (alama 5)

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**SEHEMU YA C**

**Tamthilia:** *Kigogo* **-** Pauline Kea

Jibu swali *4* au *5*

**4.** Mwandishi wa tamthilia ya *Kigogo* amefanikiwa katika kutumia ishara ili kufanikisha maudhui. (alama 20)

**5.** Mimi sili makombo kama kelbu! Nilishakunywa chai ya mke wangu nikaridhika."

(i) Eleza mkutadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Fafanua mtindo katika dondoo hili. (alama 4)

(iii) Jadili vile Wanasagomoyo wamefanywa kelbu kula makombo (alama 12)

**SEHEMU D**

**Hadithi Fupi:** *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* - Chokocho Na D. Kayanda:

Jibu swali la *6* au *7*

**6.**

i) Tathmini umuhimu wa Samueli Matandiko Katika kuijenga hadithi, "Mtihani wa Maisha" (alama 10)

ii) Fafanua shibe inavyomaliza Waafrika katika hadithi ya "Shibe Inatumaliza". (alama 10)

"Tulipokutana Tena" - Alifa Chokocho.

**7**. ***a)*** 'Jijini ni kuzuri. Kuna majumba makubwa, utapanda magari mazuri mazuri ya marafiki zetu, utakula vyakula vitamu na kupewa nguo za fahari. Utapelekwa shule kusoma na kwandika.'

i) Jadili muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii) Eleza taswira zinazojitokeza katika dondoo hili kwa kutoa mifano. (alama 3)

iii) Aliyoambiwa msemewa ni kinyume cha yaliyotokea. Eleza. (alama 8)

**b)** Wahusika mbalimbali katika hadithi hii wanatumia njia nyingi kukabiliana na matatizo yanayowakumba. Zijadili.

(alama 5)

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**SEHEMU YA E**

**Fasihi Simulizi**

Malaika …..

Nakupenda malaika x 2

Ningekuoa mali we…..

Ningekuoa dada…..

Nashindwa na mali sina we…..

Ningekuoa malaika x 2

Pesa, zasumbua roho yangu x 2

Nami nifanyeje, kijana mwenzio

Nashindwa na mali sina we

Ningekuoa malaika x 2

i) Tambua utungo huu. (alama 2)

ii) Toa sababu za jibu lako hapo juu (alama 2)

iii) Taja shughuli ya kijamii na shughuli ya kiuchumi inayodokezwa kwenye kipera hiki. (alama 2)

iv) Tambua nafsi neni na nafsi nenewa. (alama 2)

v) Jadili vipi mwasilishji wa kipera hiki anaweza kuboresha wasilisho lake.(alama 6)

vi) Ni matatizo yapi yanayoweza kumkumbuka mkusanyaji wa kipera hiki nyanjani? (alama 6)

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources